# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 8 Juni, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. David K. Mwakiposa) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:** Maswali.

### MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi Mbunge wa Jimbo la Mlalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naamini na wewe leo umeingia katika historia ya kuongoza Bunge la wanaume pekee. *(Makofi)*

Na. 387

### Upungufu wa Walimu – Lushoto

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Halmasauri ya Wilaya ya Lushoto ina upungufu wa walimu wa shule za msingi takribani 1,270 kwa mujibu wa ikama.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka walimu katika Halmashauri hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Jimbo la Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 2019/2020 Serikali imeajiri na kuwapanga walimu 148 wa shule za msingi na walimu 118 wa shule za sekondari katika Halmashauri ya Lushoto kati ya walimu 26,181 wa shule za msingi na sekondari walioajiriwa katika kipindi hicho. Aidha, Serikali inaendelea kuratibu zoezi la kuajiri walimu 6,949 kwa nafasi za ajira zilizotangazwa mwezi Mei, 2021 ambao watapangwa kwenye shule mbalimbali zikiwemo za Wilaya ya Lushoto, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa sasa Serikali ipo katika mchakato wa ajira hizi mpya ambazo amezitaja 6,979 hivi na sisi upungufu wetu ni walimu 1,270.

Je, haoni sasa kuna umuhimu angalau Halmashauri kama ya Lushoto ikapewa kipaumbele angalau kwa kusogeza hata kupata walimu japo 200?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa wapo walimu ambao asili yao ni Lushoto na Tanga kwa ujumla na wapo katika maeneo mbalimbali ya nchi hii na hawa wapo tayari kurudi Lushoto kuungana na wananchi wa Lushoto

katika kutoa huduma hii ya elimu lakini changamoto za uhamisho ndio zinazowakwamisha.

Je, Serikali iko tayari kushirikiana na mimi kuwabaini wale wote ambao wapo tayari kurudi Lushoto ili kwenda kusaidia jukumu hili na kuondoa huu uhaba mkubwa wa walimu katika Halmashauri yetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS . TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ni kweli kwamba katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, lakini pia katika Jimbo la Mlalo kuna upungufu wa watumishi kwa maana ya walimu na Serikali kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi imeendelea kuwaajiri kwa awamu walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto. Naomba nimhakikishie kwamba katika ajira hizi 6,900 ambazo zinakwenda kutolewa hivi sasa ambapo tayari taratibu za kuwa-*shortlist* na kuwapata walimu hao zinaendelea, tutakwenda kuhakikisha tunampa kipaumbele cha hali ya juu sana Mheshimiwa Shangazi na Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kwa ujumla wake. Kimsingi namhakikishia kwamba tutaendelea kulifanyia kazi kwa karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; walimu wenye asili ya Lushoto ambao wanapenda kurudi kufanya kazi katika Halmashauri hiyo, utaratibu wa Serikali uko wazi na walimu na watumishi wote kote nchini wanaruhusiwa kufanya kazi sehemu yoyote, lakini wale ambao wana sababu za msingi za kuomba kurudi katika Halmashauri yoyote ile ikiwemo Lushoto bila kujali wanatokea ama hawatokei Lushoto wanaruhusiwa kufuata taratibu za Serikali za kuomba uhamisho na sisi kama Serikali tuna vigezo ambavyo

tutavitazama na kuona walimu wale wanapata vibali vya kuhama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie kwamba kama wapo wanaohitaji tunawakaribisha, lakini kwa kufuata vigezo na taratibu zile za Serikali, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya tunaendelea na Wizara ya TAMISEMI, sasa aulize swali Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Kwa niaba yake mimi hapa Stanslaus Nyongo.

**MWENYEKITI:** Haya endelea.

Na. 388

**Elimu ya Ujasiriamali kwa Wanawake na Vijana Wanaopata Mikopo Asilimia Tano katika Halmashauri**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO K.n.y. MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wanawake na vijana katika Halmashauri wanapewa mikopo ya asilimia tano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, karibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 23 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya asimilia 10 kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka 2019, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kutoa mafunzo kwa vikundi vilivyokubaliwa kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Kanuni hiyo Serikali ilikwishaanza kutoa elimu ya ujasiriamali na katika mwaka wa fedha 2019/2020 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetoa mafunzo kwa vikundi 11,915 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambavyo vilipewa mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri zote nchini. Mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na mafunzo ya ujasiriamali, utunzaji fedha, uendeshaji na usimamizi wa miradi, utoaji taarifa na usimamizi wa marejesho ya mikopo. Serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa itaendelea kutoa elimu kwa vikundi hivyo ili kuvijengea uwezo wa kuendelea kukua na kutumia ipasavyo fursa mbalimbali za kiuchumi katika maeneo yao, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza fedha hizi zimekuwa zikitolewa na Halmashauri, lakini hatuoni ni namna gani zinavyorudishwa ili kuweza kukopeshwa watu wengine; je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inaweka mkakati thabiti wa kuhakikisha kwamba hizo fedha zinavyorudi basi wapewe na watu wengine ili waweze kupatiwa mikopo hiyo na kuweza kujiendeleza katika biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kutoka kwenye asilimia nne kwa wanawake, nne kwa vijana na mbili kwa walemavu kuongeza asilimia walau ziwe 15 ili kila kundi lipate asilimia tano tano? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba fedha hizi asilimia kumi ambazo zimekuwa zinatolewa kwa vikundi vya wajasiriamali katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa zimewekwa kwa mujibu wa sheria na kKanuni ili ziwe ni fedha ambazo zinazunguka kwa maana ya *revolving fund.* Kwa maana kila vikundi ambavyo vinakopeshwa vinapaswa kutekeleza shughuli hizo za ujasiriamali na kurejesha fedha zile ambazo zilikopwa bila riba yoyote ili ziweze kutumika pia kuwakopesha vikundi vingine na hatimaye kuendelea kuwajengea uchumi mzuri wana vikundi katika vikundi hivi vya ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto ya urejeshaji wa fedha hizi kwenye baadhi ya vikundi vya ujasiriamali vinavyokopeshwa. Na sheria ya sasa imeweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba tunakwenda kufungua akaunti maalum kwa ajili ya fedha hizi za mikopo ya asilimia kumi na kuhakikisha kila kikundi cha ujasiriamali kitarejesha fedha hizo na zionekane zinarejeshwa na kukopeshwa kwenye vikundi vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwaelekeza Wakurugenzi wote wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhakikisha wanalisimamia kwa karibu sana suala la mikopo na marejesho na sisi kama Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Serikali kwa ujumla tutakwenda kufanya kaguzi kuona fedha zilizokopeshwa zinarejeshwa na zinaendelea kukopeshwa katika vikundi vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; tumeweka asilimia kumi kutokana na mazingira ya fedha za mapato ya ndani kuwa yana majukumu mengi sana; sote tunafahamu asilimia 40 kwa

ajili ya miradi ya maendeleo, asilimia 60 kwa Halmashauri za Mijini kwa ajili ya miradi ya maendeleo, lakini pia kuna shughuli zingine nyingi. Wazo hili ni zuri la kufikiria kuongeza asilimia 15 lakini tutakwenda kulifanyia tathmini na kuona kama linawezekana kutekelezwa lakini kwa sasa tunaendelea na asilimia kumi kwa sababu tumeangalia vigezo mbalimbali ili kuziwezesha Halmashauri kuendelea na shughuli zake. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Haya tunakwenda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake namba 389.

Na. 389

**Askari Polisi Kupewa Nafuu ya Kodi, Vifaa yya Ujenzi na Viwanja**

**MHE. OMAR ALI OMAR K.n.y. MHE. AGNESTA L. KAIZA** aliuliza:-

Je ni kwa nini askari polisi wasiwekewe utaratibu wa kusamehewa kodi katika vifaa vya ujenzi na kupewa viwanja kwa bei elekezi ili wawe na moyo wa kulitumikia Taifa bila kujiingiza katika njia za udanganyifu kwa lengo la kujiandaa na maisha baada ya kustaafu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri karibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa utoaji wa msamaha wa kodi kwa bidhaa mbalimbali vikiwemo vifaa vya ujenzi kwa askari wa Jeshi la Polisi ulikuwa unatekelezwa kupitia Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* na

kutokana na changamoto za kimuundo na mfumo uliosababisha uvujaji wa mapato na utozaji kodi usio na usawa, Serikali ilifanya marekebisho yaliyopelekea kufutwa kwa baadhi ya misamaha ya kodi ikiwemo ya vifaa vya ujenzi kwa vyombo vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua kazi kubwa na nzuri katika kulitumikia Taifa letu inayofanywa na vyombo vya ulinzi na usalama ikiwemo Jeshi la Polisi, ilianzisha utaratibu mwingine wa kibajeti wa kutoa nyongeza ya posho maalum kwa kila Askari ili kufidia gharama za kodi pale wanapofanya manunuzi ya vifaa vya ujenzi pamoja na mahitaji yao mengine. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omar Ali Omar, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba posho ya shilingi 100,000 ambayo ilikuwa inatolewa kwa ajili ya kuwawezesha askari wetu waweze kukidhi haja ya kuweza kujenga, tukiangalia kwa mtazamo ni kwamba posho hiyo ilikuwa ni ndogo na hata askari wakipewa miaka 100 hawawezi kufanya ujenzi kwa posho hiyo.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwawezesha askari wetu kuwaongezea posho hii ili iendane na utaratibu wa kuweza kujenga kwa askari wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba mbili; je, sasa Serikali haioni kwamba kuna haja kwa Wizara kuhakikisha kuona kwamba pamoja na kwamba askari wetu wanaintelijensia ya hali ya juu, hatuoni sasa kwamba kuna haja sasa ya ule utaratibu wa mwanzo kuweza kutumika ili kwamba askari wetu tuweze kuwaweke katika mazingira mazuri waweze kulinda nchi hii, raia pamoja na mali zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba sasa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar Ali Omar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ipo tayari ama ina utaratibu gani sasa wa kuongeza hii posho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo dhamira kwa sababu kwanza nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba vyombo vyetu vya ulinzi hasa Jeshi la Polisi wanafanya kazi nzuri na kwa kweli tunayo kila sababu ya kuwatengenezea mazingira mazuri ya kuendelea kufanya kazi vizuri, katika hili tunawapongeza sana. Kikubwa ni kwamba utaratibu wa kuongeza hizi posho upo, tumeshaupanga/tumeshaufikiria maana hata katika bajeti ambayo tuliiwasilisha juzi tulilizungumza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa nimwambie tu Mheshimiwa awe na stahamala kwa sababu hii mipango inahitaji fedha na tupo mbioni kuhakikisha kwamba tunatafuta hizo fedha ili tuweze kuwaongezea kwa sababu hatuwezi tukasema kwamba kesho tutawaongezea, kwa hiyo, kesho watazipata lakini *the way* ambavyo kasungura ketu kananenepa ndivyo ambavyo tutakapokuwa tunawaongezea na wao hii posho ili sasa waendelee kufanya kazi nzuri zaidi ya kulinda raia na mali zao. Kwa hiyo, hiyo nia ya kuwaongezea posho ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini je, hakuna haja ya kurejesha ule utaratibu wa mwanzo, mimi nadhani Mheshimiwa Mbunge atupe nafasi tuende tukakae na wenzetu tukalifikirie hili, tukapange halafu tutaona sasa namna bora ya kuboresha haya mambo ili sasa kuweza kurejesha ule utaratibu wa mwanzo ambao kama yeye Mheshimiwa Mbunge ameuzungumzia. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, karibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri Khamis, lakini nataka nikubaliane na muuliza swali la msingi Mheshimiwa Lambert pamoja na maswali yake ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ni kweli tunakubaliana kwamba vijana hawa askari polisi wanafanya kazi nzuri kwa nchi na Taifa lao na pengine wanafanya hivyo katika mazingira magumu na wengine kulingana na vyeo vyao ni vigumu sana kujikomboa na kupata hata maisha mazuri baada ya kumaliza utumishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lililosemwa katika swali la msingi ni kama je, Serikali haioni haja ya kuwapatia vijana hawa viwanja kwa bei nafuu? Nataka niseme sisi kama Wizara tunalichukua hili, tutajadiliana na wenzetu wa Wizara ya Ardhi tuone uwezekano huo kwa sababu ni jambo jema kabisa na wengine kweli wanamaliza/wanastaafu wakiwa kwanza na umri mdogo kulingana na Kariba ya ajira yenyewe ya Jeshi la Polisi, mtu ana miaka 54 anastaafu, halafu hana hata nyumba wala kiwanja. Nataka nikubaliane kwamba acha tulifanyie kazi, tuone kwa mfumo ambao uliopo kama tunaweza tukawapatia vijana hawa angalau viwanja, angalau kwa wale wa vyeo fulani fulani ambao unajua wapo kidogo *underprivileged.* Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, mmezungumzia upande wa viwanja nafikiri pia Serikali mtajipanga na hoja ya pili ya muuliza swali ameuliza mambo mawili; msamaha wa kodi katika vifaa vya ujenzi pamoja na viwanja kwa bei elekezi. Kwa hiyo, nafikiri..., karibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tulikuwa na utaratibu wa *duty free shops* kwa ajili ya hawa askari. Maduka haya yalitumika na ukatokea ukiukwaji mkubwa sana wa taratibu za kikodi na kutokana na mazingira hayo mambo mengi mabaya

yalitokea, Serikali ikaona bora kuondoa ile kwa sababu waliokuwa wananufaika ni watu fulani, fulani tu hata walengwa pengine walikuwa hawanufaiki, tukaona bora waingiziwe fedha zao na kwa utaratibu wa sasa wanalipwa shilingi 300,000 kila baada ya miezi mitatu, ni kitu fulani kuliko wengine ambao walikuwa vijijini huko hata *duty free shops* hizo hawazioni. Na utaratibu huo wa ku-*institutionalize* leo ni vigumu sana. Kwa hiyo, utaratibu wa fedha kuingizwa kwenye akaunti zao umekuwa ni bora na wanaufurahia sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa majibu mazuri. Tunakwenda Wizara ya Kilimo sasa namuita Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya na swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama kwa niaba yake.

Na. 390

**Kuweka Miundombinu ya Umwagiliaji- Bonde la Mto Ruhuhu**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA K.n.y. MHE. ENG.STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Bonde la Mto Ruhuhu lililopo Kata ya Lituhi linawanufaisha wananchi kwa kuweka miundombinu ya Kilimo na umwagiliaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Jimbo la Nyasa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Bonde la Mto Ruhuhu linalojumuisha sehemu ya Wilaya Ludewa Mkoni Njombe na Wilaya ya Nyasa Mkoani Ruvuma

linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Upembuzi yakinifu wa awali kuhusu kilimo cha umwagiliaji katika bonde hili ulifanyika mwaka 2013/2014 na kubaini uwezekano wa kujenga bwawa kubwa; matumizi mbalimbali ikiwemo kilimo cha umwagiliaji kwa takribani hekta 4,000 na kufua umeme wa megawati 300. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania linaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Bwawa la Kikonge lililopo ndani ya Bonde la Mto Ruhuhu kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na uendelezaji wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji chini ya Bwawa la Kikonge.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu itakapokamilika na kutathimini gharama halisi, Serikali itatafuta fedha za ujenzi wa bwawa hili pamoja na fedha za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji chini ya Bwawa la Kikonge ili kuongeza uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo katika eneo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Mhagama, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Mkoa wa Ruvuma umejaaliwa kuwa na mito mingi mikubwa, mito hiyo ipo pia katika eneo la Jimbo la Madaba moja katika mito mikubwa ni mto huo Ruhuhu, lakini kuna Mto Hanga.

Nini sasa mkakati wa Serikali kuhakikisha maeneo hayo yote yanayofaa kwa umwagiliaji tunakuwa na miundombinu mikubwa na rafiki itakayoboresha kilimo cha mpunga na kilimo cha umwagiliaji katika ujumla wake maeneo ya Mkoa wetu wa Ruvuma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mhagama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali sasa hivi tunachokifanya ni kufanya *review* ya *master plan* yote ya umwagiliaji na kubadili mfumo wa Tume yetu ya Umwagiliaji ili kuweza kupata tija katika miradi yetu ya umwagiliaji na kuwa na gharama ambazo ni *affordable* na kuna *value for money,* hili ni jambo la kwanza.

La pili tunachokifanya sasa hivi tutatambua maeneo ya kimkakati ambayo Serikali itaenda kuwekeza yenyewe 100% na maeneo mengine ya umwagiliaji tuta-*encourage* sekta binafsi kuweza kufanya hayo maeneo na kuwekeza sekta binafsi kwa makubaliano ya *long term* ili kupunguza mzigo. Kwasababu siyo lazima kila sehemu ndiyo Serikali iweze kujenga yenyewe. Kwa hiyo, tunafanya jitihada za namna hiyo kuweza kuzi-*cruster* hii miradi ya umwagiliaji katika maeneo ambayo itawekeza sekta binafsi na maeneo ambayo Serikali itakwenda kuwekeza kwenye miradi mikubwa ambayo sekta binafsi haiwezi kuwekeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deus Sangu, Mbunge wa Kwela, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imeanza kuwekeza fedha za awali katika *scheme* za umwagiliaji kama *scheme* ya Ilemba, Ng'ongo, Sakalilo, Mititi na Bonde la Ilembo; ni lini Serikali itapeleka fedha kumalizia hizi *scheme* ambazo tayari imeanza na ipo katika mipango yake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza *priority* namba moja katika bajeti ya mwaka huu tunayoanza nayo ni kukamilisha

*scheme* ambazo tulishapeleka fedha na ambazo hazijakamilika. Kwa hiyo, *scheme* zote zipo karibu 1000 na kidogo ambazo zimepelekewa fedha nusu/nusu hazijakamilika. Kwa hiyo, hii ni *priority* ya kwanza.

Kwa hiyo, nimuhakikikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kote ambako tulishapeleka fedha na kuanza kuzifanyia kazi, tunafanya tathmini ya mapungufu yaliyopo na ukamilishaji, kwa sababu zipo *scheme* ambazo tulienda kujenga mifereji wakati hatujatengeneza bwawa la kuweza kuhifadhi maji, kwa hiyo, ni *wastage of resources*. Kwa hiyo, tunafanya hiyo tathmini na kuitambua na tuta-*communicate officially* kwa Wabunge kila mmoja kuweza kufahamu *scheme* zake zilizoko kwenye eneo lake ni lini zitaanza kufanyiwa kazi na zipo kwa sababu tuna-*resource* ndogo, tutapeleka *scale of preference* na kuchagua zipi tunaanza nazo kuweza kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *priority* ya pili ya bajeti yetu ya mwaka huu kwenye fedha tulizotenga ni kuwekeza fedha kwenye mashamba 13 ya kuzalisha mbegu ili tuondokane na tatizo la mbegu katika nchi kwa sababu tuna mashamba ya kuzalisha mbegu, lakini hatujawekea miundombinu. Serikali inakwenda shambani kuandaa mbegu wakati ambapo mkulima naye yupo shambani. Kwa hiyo, ni jambo la aibu, tumeamua kwamba *resource* tunaweka namba moja kwenye mbegu; namba mbili kukamilisha *scheme* ambazo tulipelekeka fedha kidogo kidogo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakwenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Sasa namwita Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale.

Na. 391

**Ujenzi wa Chuo cha Veta – Liwale**

**MHE. ZUBERI M. KACHAUKA K.n.y. MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, Serikali iko tayari kuunga mkono juhudi za wananchi wa Kata ya Makata - Liwale ambao wameanzisha ujenzi wa Chuo cha *VETA* na madarasa mawili yamekamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kachauka, Mbunge Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua jitihada zinazofanywa na wananchi za kuona umuhimu wa kuwa na Chuo cha Ufundi Stadi katika maeneo yao wakiwemo wananchi wa Kata ya Makata - Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Serikali ni kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Wilaya nchini. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali inaendelea na ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya 29 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inaendelea na mpango huu kwa awamu, nashauri wananchi wa Kata ya Makata waendelee na juhudi hizo wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha. Aidha, niombe uongozi wa Wilaya ya Liwale uwasiliane na uongozi wa *VETA* kuweza kuona namna ya kupata msaada wa kitaalam kuhusu ujenzi wa majengo ya Vyuo vya Ufundi Stadi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu haya ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale.

Swali la kwanza, je, Serikali inatuahidi nini katika bajeti ijayo?

Lakini swali la pili; je, Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri atakuwa tayari kwenda kuona juhudi za wananchi Liwale lakini wakati wa kwenda au wa kurudi apitie Kilwa Masoko kwa ajili ya kuona changamoto zilizopo katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kassinge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ijayo kwasababu tuna ujenzi wa vyuo hivi 29 katika Wilaya 29 nchini. Katika bajeti ijayo tumepanga kununua vifaa ambavyo vitakavyowezesha sasa vyuo hivi ifikapo Januari, 2022 viweze kuanza kutoa huduma kwa maana kwamba vianze kutoa huduma ya kufundisha wanafunzi katika maeneo hayo. Hilo ndio lengo letu katika bajeti ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili suala la pili la kuweza kwenda kuona maeneo haya nipo tayari, baada ya Bunge hili la Bajeti tutapanga ziara na hata jana tulikuwa na uwekeaji wa jiwe la msingi katika chuo chetu cha *VETA* pale katika Wilaya ya Ruangwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pamoja na maeneo mengine na dhamira ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba nafika Liwale, lakini nitafika Ruangwa, lakini vilevile nitafika kwa ndugu yangu Kassinge pale Kilwa Kusini kuweza kuona changamoto zilizopo na kwa namna gani ya kuweza kuzitatua. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Festo Sanga swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Swali langu lilikuwa, kwanza niwapongeze Makete tumepata Chuo cha *VETA* ambacho kwa Mkoa mzima wa Njombe kipo Makete tu. Lakini tuna changamoto ya kozi ambazo mnazitoa pale nyingi hazipo kwenye soko kwa mfano; hatuna kozi ya ufundi magari, hatuna kozi ya ufundi umeme majumbani, hatuna kozi ya ambayo inashughulikia masuala ya mabomba kwa maana ya ufundi mabomba.

Je, ni lini Serikali italeta hizo kozi ambazo kwa sasa ziko kwenye soko Tanzania kutokana na hizi ambazo tunatekeleza kwenye Ilani hasa hasa suala la umeme vijijini ambapo wana Makete wengi wangependa wafanye kazi kwenye mazingira hayo lakini kozi hizo hazipo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba nijibu swali la Mheshimiwa Sanga, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna kozi ambazo ziko *standard* karibu kwenye maeneo mengi sana na kwa sasa hivi kunaonekana kama kuna uhitaji mkubwa sana kwenye baadhi ya maeneo kwamba tubadilishe kozi kuendana na maeneo yale yalivyo. Mfano, nilikuwa kule Mwanza katika Visiwa vile vya Ukerewe hakuna kozi zinazohusiana na masuala ya uvuvi. Lakini wakasema sasa ni muhimu sana tuweze kuianzisha kozi ile. Nimtoe wasi wasi Mheshimiwa Sanga kwamba jambo hili tunakwenda kulifanyia kazi, tutakwenda kukaa na uongozi wa Mkoa na kuhakikisha kwamba kozi hizi ambazo ni muhimu, lakini vilevile zenye soko kwenye maeneo hayo zinaenda kuanzishwa mara moja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri naamini pia utachukua pamoja na Mufindi

Kusini ambako wana ardhi wangehitaji nao wapate Chuo cha *VETA* pale Kilolo.

Sasa tunakwenda Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, sasa namwita Mheshimiwa Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Ulanga aulize swali lake.

Na. 392

**Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Ifakara - Mahenge**

**MHE. DENNIS L. LONDO K.n.y. MHE. SALIM A. HASHAM** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Ifakara – Mahenge utaanza kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alaudin Hasham Salim, Mbunge wa Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** barabara ya Ifakara – Mahenge ni sehemu ya Barabara Kuu ya Mikumi, Kidatu, Ifakara, Lupiro, Mahenge/Malinyi, Kilosa kwa Mpepo, Londo hadi Lumecha yenye urefu wa kilometa 547 ambayo inaunganisha Mikoa ya Ruvuma na Morogoro. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii ilikamilika mwaka 2018 kwa lengo la kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** hadi sasa ujenzi wa Daraja la Magufuli lenye urefu wa mita 384 pamoja na barabara unganishi yenye urefu wa kilometa 9.142 umekamilika. Ujenzi

wa sehemu ya Ifakara – Lupiro – Mahenge utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami zikiendelea, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* itaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara husika ili ipitike majira yote ya mwaka. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara hii swali lilkuwa ni lini ujenzi utaanza. Lakini barabara hii haina tofauti na barabara nyingine ya kutoka Kilosa kuja Mikumi ambayo ipo kwenye Ilani ya mwaka 2015/2020, 2020/ 2025 na ipo kwenye bajeti hii ya mwaka huu na bado tunaambiwa kwama ipo kwenye maandalizi. Sasa Je, ni lini ujenzi wa barabara hii unaenda kuanza? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi ni lini? Sasa ujibu swali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nniaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Londo, Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli barabara ile aliyotaja ya Kilosa Mikumi ipo kwenye Ilani na imetengewa fedha kwa bajeti inayokuja. Kwa hiyo, tunaamini kwamba tutakapoanza utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/2022 basi hii barabara itakuwa moja ya barabara ambazo zitaendelea kujengwa kwani tayari barabara hii upande inapoanzia eneo la hapa njia panda barabara ya Morogoro – Dodoma; tayari imeshajengwa mpaka Kilosa na tunaendelea na ujenzi. Kwa hiyo kipande kilichobaki cha Kilosa kwenda Mikumi barabara hii naamini nayo itaanza kujengwa katika bajeti tunayoanza kuitekeleza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa barabara hii inayotajwa pia upo kwenye kufungua Mkoa wa Lindi na kwa ajili ya uchumi wa Kusini. Lakini Serikali mara nyingi imekuwa ikiongea tu kuhusu eneo hili la kusahau *junction* inayoanzia maeneo ya Mbingu kule Ifakara inapita Liwale inakwenda kutokea Nachingwea mpaka Masasi na yenyewe ni muhimu kama ilivyo hivyo.

Sasa Serikali itueleza hapa kwa sababu tulikuwa tukiongea kuhusu barabara hii mara nyingi kwamba ni lini sasa pamoja na nia njema ya kutaka kutengeneza hii barabara inayokwenda Ruvuma mtamalizia na ile *junction* inayokuja kutokea Liwale kuja Nachingwea mpaka Lindi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwambe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja kuanzia Mbingu, Liwale hadi Nachingwea ni barabara ambayo kweli ipo imeahidiwa lakini ujenzi wa barabara hii utategemea na upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, kwanza itatakiwa ifanyiwe upembuzi na baadaye usanifu wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumepitisha bajeti, kwa hiyo, itategemea na upatikanaji wa fedha ambayo kama itapatikana fedha basi miradi hii itaanza kutekelezwa sawasawa na miradi mingine. Lakini kikubwa ni ufinyu wa bajeti ambao unafanya barabara hizi zote haziwezi kutekelezwa kwa wakati mmoja. Lakini ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa ili kuweza kufungua maeneo haya na pia kupunguza umbali ambao wananchi wanasafiri kuzungukia barabara ambazo ni ndefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita katika wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi aulize swali lake.

Na. 393

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege - Singida**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Singida ili ndege za *ATCL* zianze kutua na kurahisisha usafiri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanja cha ndege cha Singida ni miongoni mwa viwanja 11 vilivyofanyiwa Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ufadhili wa fedha kupitia mradi wa Benki ya Dunia. Viwanja hivyo 11 ni kama ifuatavyo; *Lake Manyara,* Musoma, Songea, Kilwa Masoko, Tanga, Iringa, Lindi, Moshi, Singida, Njombe na Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hatua ya awali ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kukamilika, Serikali imejipanga kuanza hatua ya ujenzi kwa viwanja vyote vya ndege kwa awamu kwa kutumia fedha za ndani kutokana na ukweli kwamba gharama za ujenzi wa viwanja hivyo ni kubwa ukilinganisha na bajeti inayotolewa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia bajeti, Serikali kupitia *TANROADS* imejipanga kuanza na ujenzi wa viwanja

vya Iringa na Songea. Ujenzi wa viwanja vilivyobaki kikiwemo cha Singida utaanza mara Serikali itakapopata fedha. Aidha, kwa sasa Serikali inaendelea kuwasiliana na washirika wa maendeleo ili kuweza kupata fedha za kujenga viwanja hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo hapo juu, namuomba Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu na wananchi wa Singida waendelee kuvuta subira kwani Serikali ya Chama cha Mapinduzi ina nia ya dhati ya kujenga kiwanja hicho cha Singida. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Elibariki Immanauel Kingu, swali la nyongeza.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza pia kukuona umekaa kwenye hicho kiti kwa kweli kimeku-*fit* sawasawa. Kama Mbunge kijana nakupongeza sana, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la nyongeza ni kwamba imekuwa ni habari kwa kweli ya muda mrefu sana, wananchi wa Mkoa wa Singida tumeendelea kupata ahadi, ahadi, ahadi ambazo kwa kweli kimsingi ningependa sana kaka yangu na mtani wangu ninaye muheshimu sana watupe *commitment* kama Serikali; uwanja huu wa ndege wa Mkoa wa Singida. ambao kimsingi tuko jirani kabisa na Makao Makuu ya nchi lini Serikali inakwenda kuanza ujenzi wa uwanja huu kwa maslahi ya wananchi wa Mkoa wa Singida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nipate *commitment. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, *commitment,* kwa ufupi sana.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa

Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Immanuel Kingu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika ujenzi wa uwanja wa ndege au kama ilivyo kwenye barabara tayari uwanja huo umefanikiwa kupata hatua ya kwanza. Tumesema usanifu na upembuzi yakinifu umeshafanyika; maana yake tayari hapa tulipo tunajua angalau inahitajika gharama kiasi gani. Tunatafuta mapato ya ndani, lakini pia na washirika wetu wa maendeleo. Tukipata fedha hata kesho Mheshimiwa Kingu, uwanja huu utaanza kujengwa.

Naomba nikuhakikishie kwa niaba ya Serikali kwamba tuna nia ya dhati kwamba kila Makao Makuu ya Mkoa kuwe na uwanja wa ndege ili uweze kutoa huduma katika maeneo yale. Kila Mheshimiwa Mbunge angeweza kupenda baada ya Bunge kuahirishwa apande ndege itue nyumbani kwake kwenye mkoa wake, achangie mapato, lakini pia na wageni wengine wapate huduma kirahisi sana. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simon Songe, Mbunge wa Busega swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa uhitaji wa uwanja wa ndege Mkoa wa Singida ni sawa na uhitaji wa uwanja wa ndege Mkoa wa Simiyu na tumekuwa tukipata majibu kwamba Serikali iko kwenye mchakato.

Sasa na mimi nataka tu *commitment* kwamba je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa uwanja wa ndege Mkoa wa Simiyu pale Igegu ili wananchi waweze nao kupanda ndege nikiwemo na mimi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa

Ujenzi na Uchukuzi ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye swali la Mheshimiwa King una kwa kuwa mkoa huu ni mkoa mpya, Mkoa wa Simiyu na usanifu wa kina na upembuzi yakinifu umeshafanyika, gharama zimeshajulikana, Serikali inatafuta vyanzo mbalimbali, tukipata fedha Mheshimiwa Mbunge wa Busega naomba nikuhakikishie kwamba utapata uwanja katika Mkoa wa Simiyu. Kama ambavyo ameanza mapema lakini wanafanya kubwa sana. Hongereni sana kwa kazi nzuri ambayo mnafanya katika mkoa huo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona; kwa kuwa Mkoa wa Njombe nao ni mkoa mpya na kwa kuwa uwanja wa ndege upo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kwa kuwa Njombe tumekuwa tukilima sana maparachichi.

Swali, ni lini Serikali itaanza kutekeleza kuujenga uwanja wa ndege katika Mkoa wa Njombe na kwa sababu Mbunge amekuwa akiuliza mara nyingi sana Mbunge Mwanyika juu ya uwanja wa ndege? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa swali hili lenye maslahi kwenye maparachichi ambayo ni *green gold.*

**NAIBU WAZIRI, UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge mzoefu na maarufu katika Bunge hili tukufu; ni kweli kwamba Mkoa huu ni mkoa mpya na ni maarufu kwa kilimo cha maparachichi ambayo pia sasa hivi yamepata soko nje ya nchi. Wanahitaji uwanja wa ndege ili maparachichi yale yatoke moja kwa moja Njombe yaende popote ambapo yanahitajika huko duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema ana bahati kwamba eneo lake hili usanifu umeshafanyika, gharama zimeshajulikana na kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais Mama Samia kwamba Watanzania walipe kodi bila shuruti, pamoja na vyanzo vingine tukipata fedha za kutosha hata kesho tutajenga uwanja huu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza kwa Wizara hii hii ya ujenzi bado.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa kuwa ipo barabara ambayo ilitolewa ahadi na hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, barabara ya Kibamba – Mpiji – Mabwepande na tayari bajeti ya Wizara hii imepita.

Sasa nataka kauli ya Serikali juu ya bajeti husika juu ya barabara hii; ni nini kimefanyika juu ya utengenzaji wa barabara hii katika mwaka huu ikitegemea Hayati alisema wapelekewe kwa udharura?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu swali hili.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba bajeti yetu imepitishwa tarehe 27 na 28 Mei, 2021 hapa Bungeni tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kupitisha bajeti yetu. Tunaomba tuwahakikishie kwamba ahadi zote za viongozi wakuu, Mheshimiwa Rais Hayati Magufuli, Mama Samia aliyepo madarakani sasa, Mheshimiwa Waziri Mkuu na ambazo zimetajwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi zitatekelezwa. Tupeane muda tu. Mheshimiwa Mbunge, tutapitia kwa haraka haraka tuweze kujua ni barabara gani zimetajwa, zipo nyingi nchi nzima. Siwezi kukudanganya hapa lakini tukipitia kama ipo na fedha yake imetengwa tutaisimamia na kazi itafanyika na bahati nzuri

tumepanga kwamba eneo hilo tutoe malalamiko mkoa wa Dar es Salaam, tumewekeza fedha za kutosha kuboresha barabara ili uchumi wa Tanzania uendelee kuku ana fedha hizo zifanye kazi za kujenga uchumi wa Watanzania kutoa huduma za kijamii. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Sasa namuita Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi aulize swali lake.

Na. 394

**Ujenzi wa Barabara ya Mianzini Ngaramtoni**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa barabara ya Mianzini, Sambasha, Ngaramtoni hadi Hospitali ya Selari kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Ole Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, aliagiza barabara ya Mianzini – Sambasha – Ngaramtoni hadi Hospitali ya Selari yenye urefu wa kilometa 18 kupandishwa hadhi ili isimamiwe na Wakala wa Barabara nchini *(TANROADS)* na aliagiza ijengwe kwa kiwango cha lami. Awali barabara hii ilikuwa inasimamiwa na Halmashauri za *Arusha DC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia agizo la Mheshimiwa Rais, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini *(TANROADS)* ilifanya usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami pamoja na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni kazi ambayo ilikamilika mwaka 2019. Zabuni za ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwa kilometa zote 18 zimetangazwa tarehe 17 Mei, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami zitaanza mara baada ya tathmini ya zabuni kukamilika na mkandarasi kupatikana. Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 jumla ya shilingi bilioni 2.5 zimetengwa kwa ajili ya mradi huu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri ambayo yanaonesha kwamba kwa kweli Serikali inafanya kazi nzuri sana, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, je, fedha ambazo kiasi kilichotengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo shilingi bilioni 2.5 zinatosha kukamilisha barabara hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Jimbo la Arumeru Magharibi mazingira yake kwa maana ya miundombinu sio mizuri kabisa. Naomba kujua je, tuna barabara mbili, barabara ya Malalua – Nduruma – Bwawani inayounganisha Simanjiro na Arumeru Magharibi na barabara ya *TPRA* – Likamba inayounganisha na Monduli.

Je, haioni sasa ni busara kwa ajili ya mazingira ya Jimbo hilo magumu barabara hizo mbili kupandishwa hadhi kupelekwa *TANROADS? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba fedha iliyotengwa haiwezi ikakamilisha kilometa 18, lakini hii ni fedha ya awali kwa ajili ya kuanza mradi na wakati huo Serikali itaendelea kutafuta fedha ili kukamilisha mradi huu. Mradi huu utaenda kwa awamu, fedha iliyopatikana tutaanza na kazi na kazi itakavyozidi kupatikana basi tutakamilisha huu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili nimshauri Mheshimiwa Noah Lemburis, Mbunge wa Arumeru Magharibi kwamba hizo barabara ambazo amezitaja kuna utaratibu maalum ambao kama barabara inatakiwa ipandishwe hadhi zipo taratibu, ziko kanuni ambazo zinapitia kwenye vyombo kuanzia Halmashauri kwenda kwenye *DCC,* kwenda Mfuko wa Barabara wa Mkoa hadi *RCC* ambao wanaleta hayo maombi kwenye Wizara yetu na sisi tunafanya tathmini na kuona inakidhi vigezo vya kupandishwa daraja ili barabara hizo ziweze kuhudumiwa na Wakala wa Barabara *TANROADS.* Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Noah uende ukafanya mchakato huo nasi tutafanya tathmini na kama zitakidhi vigezo barabara hizo zitasimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS).* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mbunge wa Mlimba swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Kwa kuwa Mkoa wa Morogoro ni Mkoa pekee nchini ambao haujaunganishwa kwa kiwango cha lami na mikoa mitatu; Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Ruvuma, na Mkoa wa Njombe.

Sasa swali langu dogo la nyongeza ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye

kilometa 223 kutoka Ifakara – Mlimba mpaka Madeke - Lupembe – Njombe? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kunambi kwa kufuatilia hiyo barabara. Mikoa aliyoitaja ni kweli barabara hazijaunganishwa kwa kiwango cha lami, lakini barabara zipo japo zinapitika kwa shida sana.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kunambi kwamba katika bajeti tunayoanza kuitekeleza atakubaliana nami kwamba Serikali imetenga fedha kuanza ujenzi wa barabara hiyo ya kuanzia Ifakara – Mlimba – Madeke mpaka *Kibena Junction* kwa kiwango cha lami.

Kwa hiyo, kwenye bajeti tunayoanza kuitekeleza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kunambi na wapiga kura wa Jimbo la Mlimba kwamba Serikali imejipanga utekelezaji kwa kiwango cha lami wa barabara hiyo utaanza. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Malima, Mbunge wa Mpwapwa swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa daraj ala Godegode linalounganisha majimbo mawili yaliyoko katika Wilaya ya Mpwapwa lilichukuliwa na maji msimu wa mvua wa mwaka 2020 na kusema ukweli uchumi wa wananchi wa Majimbo haya mawili, Jimbo la Kibakwe na Jimbo la Mpwapwa

yanategemea sana uwezo wa daraja hili, lakini pia tukizingatia kwamba daraja hili ujenzi wake uko kwenye Ilani ya Uchaguzi 2020/2025.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa daraja hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Niabu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Malima Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimuombe Mheshimiwa Malima baada ya *session* hii tuweze kuonana ili kama daraja limeondoka, kujenga daraja inaweza ikachukua muda, lakini tuna madaraja ya chuma ambayo yanaweza yakatumika kwa muda wakati Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kujenga hilo daraja kwa muda mrefu. Lakini kwa maana inaunganisha Halmashauri au Wilaya mbili nadhani itakuwa ni busara tuonane nae ili tuone na wataalam kupitia Bunge hili Mkoa huu wa Dodoma basi waende wakafanye tathmini ili tuweze kuona kama tunaweza tukajenga daraja la muda wakati tunatafuta fedha ya kujenga daraja la kudumu ili shughuli za uchumi na usafirishaji na usafiri wa wananchi ziweze kufanyika katika kipindi cha muda mfupi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Wizara hii tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mbunge wa Longido swali la nyongeza.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona na naomba nitumie fursa hii pia kukupongeza kwa Kiti hicho ulichokikalia, kwa kweli umekitendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu dogo la nyongeza linahusu ahadi ya muda mrefu sana ya barabara ya lami ambayo iliahidiwa itoke Longido mpaka Siha kuunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Kilimanjaro

kutokea Longido ambayo iko kwenye Ilani ya mwaka 2015 mpaka sasa sijajua hatua ya Serikali katika kutekeleza ahadi hiyo imefikia wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema kwenye majibu mengine barabara aliyoitaja iko kwenye Ilani na imeahidiwa na viongozi wa Kitaifa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kiruswa kwamba ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami utategemea na upatikanaji wa fedha na kadri Serikali tunavyoendelea kupata fedha nataka kukuhakikishia kwamba ni azma ya Serikali kuijenga hiyo barabara ikiwa ni pamoja na kutimizia ahadi za viongozi kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, tuvute tu subira, cha msingi tuendelee kufanya makusanyo ya fedha. Basi tutakapopata, hizo barabara zitajengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakwenda Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Sasa namuita Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, aulize swali lake.

Na. 395

**Jengo la Mama na Mtoto - Hospitali ya Rufaa ya Mawenzi**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza:-

Je, ni nini mpango wa Serikali wa kukamilisha Mradi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi ambao umeanza tangu mwaka 2008/2009 bila kukamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, sasa ujibu swali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa jengo la kuwahudumia mama na mtoto katika Hospitali ya Mawenzi umekamilika kwa asilimia 70. Mradi huo unagharimu jumla ya shilingi bilioni 10.5 ambapo hadi sasa kiasi cha shilingi bilioni 5.3 kimetolewa na kutumika.

Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 5.2 kimetengwa kwa mwaka 2021/2022 ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.6 zitatumika kukamilisha ujenzi na kiasi cha shilingi bilioni 1.6 kitatumika kununulia vifaa tiba na ujenzi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo Januari, 2022.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Umeulizwa ni lini ukajibu 2022.

Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali hii ni ya Rufaa ya Mkoa na ukisoma vitabu vya bajeti kwenye mwaka uliokwisha ilikuwa inahudumia wagonjwa karibu 75,000; mwaka huu ambao tunaumalizia wameongezeka wamefikia 96,000 na ni ongezeko la karibu asilimia 13. Lakini pia vitu vya kawaida kabisa kama nyuzi za kushona, kama *giving set,* vitu vya kawaida kabisa kwa ajili ya huduma ya akinamama havipatikani na ni Hospitali ya Rufaa.

Je, Serikali inatoa *commitment* gani kuhakikisha vitu hivi vya kawaida kabisa vinapatikana wakati tunasubiri ukamilishaji wa jingo hilo la mama na mtoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge Priscus Tarimo kwa jinsi ambavyo anafuatilia kwa umakini sio tu hospitali yetu ya Mawenzi, lakini na Hospitali ya Kanda ya Rufaa ya KCMC hasa kwenye maeneo ya miundombinu, lakini kwenye kuwatetea na kufuatilia maslahi ya watumishi wa hospitali zetu hizi zote mbili.

Swali lake ni kwamba ni lini Serikali itahakikisha kwamba vifaa vinapatikana, ametaja nyuzi na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo huko nyuma mmesikia Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan mwezi wa pili alitoa shilingi bilioni 43 kwa ajili ya vifaa tiba na dawa, lakini mwezi wan ne alitoa shilingi bilioni 80 kwa hiyo, ukijumlisha ni kama shilingi bilioni 123 zimetolewa kwa ajili ya eneo hilo la huduma ya tiba. Kikubwa ni kwamba ndani ya mwezi mmoja vifaa hivyo vitakuwa vimefika kwa sababu vimenunuliwa viwandani na hilo tatizo litakwenda kuisha na hospitali yetu itakuwa na vifaa vyote ambavyo vinahitajika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatey Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali nyingi za Halmashauri zimebaki bila kumalizika na kwa bahati mbaya Serikali imekuwa na tabia ya kupeleka fedha na mwisho wa bajeti inazichukua. Jimbo la Mbulu Vijijini hospitali imefikia asilimia 95 kumalizika.

Je, ni lini Serikali itarudisha shilingi milioni 300 ilizozichukua ili hospitali ile iweze kumalizika?

**MWENYEKITI:** Asante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tatizo ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Mbunge Massay limetokea kwenye Wilaya nyingi hapa nchini, hata ikiweko Wilaya yetu ya Siha.

Mimi ninachoweza kumwambia Mheshimiwa Mbunge tukimaliza hapa, hebu tutoke mimi na wewe twende Hazina tuangalie ni nini kimetokea na waweze kusuluhisha hilo tatizo liweze kufanyiwa kazi na fedha hizo zipatikane kazi hiyo imalizike ambayo ni asilimia tano imebaki ili hiyo hospitali ianze.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbozi lenye wakazi 300,000 halina hospitali, linategemea vituo viwili vya afya kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wake, lakini katika hivyo vituo viwili vya afya cha Itaka na Isansa havina vyumba vya kulaza wagonjwa, havina wodi za kulaza wagonjwa. Sasa pamoja na kwamba tuna madaktari wazuri wa kufanya upasuaji mkubwa katika hivyo vituo vya afya wananchi wanakosa huduma kwa sababu hawana vyumba vya kulaza wagonjwa.

Sasa nini mkakati wa Serikali wa kujenga wodi za kulaza wagonjwa kwenye hivyo vituo vya afya viwili vya Itaka na Isansa ambavyo vinategemewa katika Jimbo la Mbozi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwenye Hospitali yake ya Wilaya ya Mbozi kwanza miundombinu ni michache, lakini sasa hivi ndio inatumika kama Hospitali ya Mkoa na sasa tumeshamalizia majengo ya Hospitali yao ya Mkoa. Kwa hiyo, mzigo ulioko kwenye Hospitali ya Wilaya ya Mbozi ambao ilikuwa inaubeba kama Hospitali ya Mkoa sasa utahamia kwenye hospitali ya mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni kweli kwamba ili kuboresha huduma na kupunguza adha ya wananchi kufuata huduma mbali ni vizuri vituo vya afya viweze kusimamiwa. Kwa hiyo, mimi nafikiri Mheshimiwa Mbunge ni tukitoka hapa Bungeni tukae mimi na wewe, ili uweze kuleta vituo vya afya ambavyo umevifikiri tuangalie kama tayari tumeviingiza kwenye bajeti, kama hatujaingiza tutaweza kuingiza kupitia *Global Fund* ili viweze kufanyiwa utekelezaji.

**MWENYEKITI:** Tutamalizia na swali nyongeza kutoka kwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi narejea kwenye lile swali la msingi la Hospitali ya Mawenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Hospitali ya Mawenzi ilipandishwa hadhi ikawa Hospitali ya Rufaa na kule Moshi hakuna Hospitali ya Wilaya. Ni lini Serikali itatujengea Hospitali ya Wilaya ili iweze kuhudumia watu wa Jimbo la Moshi Vijijini, Jimbo la Vunjo na Manispaa ya Moshi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali la Mheshimiwa ndugu yetu, Profesa Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wilaya ya Moshi Vijijini haina hospitali ya wilaya na ndio maana hata baadhi ya *ambulance* kwa ombi la Mbunge ambazo zilikuwepo pale Mawenzi zimetolewa zikapelekwa kwenye vituo vya Moshi Vijijini ili kusaidia wananchi kutokana na hiyo adha ambayo anaisema.

Mimi nafikiri Mheshimiwa Mbunge kuna umuhimu wa kukaa sasa na kuangalia jiografia ya Moshi Vijijini kwa sababu ukiiangalia jiografia yake kwanza ni milimani, lakini imezunguka Mji wa Moshi Mjini; muangalie sehemu nzuri kijiografia ambayo inafaa halafu hatua stahiki zianze kufuata sasa kuanzia kwenye Halmashauri yenu kuja Mkoani - *RCC,* ili iweze kufika TAMISEMI na mwisho wa siku kazi hiyo iweze kufanyika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Tunawashukuru kwa kuuliza maswali mafupi ambayo yanatoa fursa kwa wachangiaji kuweza kuwa wengi zaidi.

Wageni naomba nitumie nafasi hii sasa kukaribisha wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; kuna wageni watatu wa Mheshimiwa David Kihenzile ambaye ndiye ninayezungumza hapa, ambao ni Spika wa Bunge la Vijana Jumuiya ya Afrika Mashariki Ndugu Hellen Mollel; Mwenyekiti wa Bunge la Vijana Jumuiya ya Afrika Mashariki Ndugu James Magumba na Ndugu Ali Chombo, Mjumbe wa Bunge hilo, karibuni sana. *(Makofi)*

Wamekuja kwa ajili ya kujifunza tunavyofanya shughuli zetu hapa Bungeni kwa sababu na wao wana Bunge lao la Vijana la Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki, karibuni sana. *(Makofi)*

Lakini pia, tunao wageni wengine wawili wa Mheshimiwa Kihenzile ambao wanatoka Wilaya ya Mufindi wakiongozwa na Ndugu Silas Simon au Kaka Meneja, naomba msimame, pamoja na Baraka Mwakipesile. Huyu Baraka Mwakipesile kwa wale mliokuwa mnafuatilia huko

nyuma ndiye aliyekuwa anamuigiza Hayati Rais Magufuli, alikuwa anaitwa Magufuli. Tunawashukuru sana, karibuni sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Lakini pia tunao wageni nane wa Mheshimiwa Mwita Waitara Mbunge na Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Wilson Rucho, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 34 wa Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo ambao ni Walimu Wakuu kutoka Halmashauri ya Jiji la Arusha wakiongozwa na Ndugu Batilda Maro na Mwalimu Ridhiwani. Batilda Maro uko wapi, kiongozi wao na Mwalimu Ridhiwani? Asanteni sana, karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 61 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Mary Hassan. Karibuni sana. *(Makofi)*

Lakini Waheshimiwa Wabunge tunao wageni wengine 20 wa Mheshimiwa Pauline Gekul Mbunge, Naibu Waziri Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, ambao ni waandaaji na wasanii wa tamasha la muziki wa dansi la kizazi kipya kutoka Mjini Dodoma wakiongozwa na mratibu wa tamasha Ndugu Kenedy Festo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wawili wa Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mbunge, ambao ni Maafisa wa Benki ya Stanbic Tawi la Dodoma wakiongozwa na Ndugu Henry Igolola na Ndugu Bakari Msuya, karibuni sana wenzetu kutoka Benki ya Stanbic. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge, ambao ni wanakwaya ya *Winners Gospel Singers* wakiongozwa na Mchungaji Mapopo, karibuni sana watumishi wa Mungu, tunawashukuru sana kututembelea. *(Makofi)*

Tunao wageni 35 wa Mheshimiwa Mohamed Monni, Mbunge, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Daudi Kitiku, wageni wa Mheshimiwa Moni hao Mbunge wa Chemba, karibuni sana tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Wengine wageni wawili wa Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge, Ndugu Witness Kachege na Ndugu Tressor Mwangaile. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Aloyce Kamamba, Mbunge, ambao ni ndugu na marafiki zake kutoka Kakonko, Mkoa wa Kigoma, wakiongozwa na Ndugu Sosthenes Katwale, karibuni sana wageni wetu kutoka Kakonko. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine saba wa Mheshimiwa Joseph Mhagama, Mbunge, ambao ni Diwani na Wenyeviti wa Vijiji vya Madaba wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Gumbiro, Mheshimiwa Gustav Tindwa. Tunashukuru sana Mheshimiwa Diwani pamoja na Wenyeviti, tunaamini mnaendelea kufanya kazi ya kumsaidia na kumlindia kura zake Mheshimiwa Joseph Mhagama. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Daimu Mpakate, Mbunge, ambao ni watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Ndugu Norbert Chale, Ndugu Aseo Ngurume na Ndugu Said Omar, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Mpakate. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Boniphace Getere, Mbunge, ambao ni wapiga kura wake kutoka Bunda Mkoa wa Mara; wageni hao ni Ndugu Leonard Kimweri yuko pale mnamuona mpiga kura wa Mheshimiwa Getere na Ndugu Rebecca Shadrack yuko pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni kumi wa Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge, ambao ni watoto wake na ndugu zake kutoka Nzuguni, Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Agape Tegete, karibuni sana, watoto wake Mheshimiwa Mwambe

wako wapi? Ahsante sana tunashukuru sana Mwalimu Tegete, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Lakini pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge, wa Makete ambao ni wafanyabiashara kutoka hapa Dodoma; wageni hao ni Yustina Mwakatobe nafikiri mnawaona wafanyabiashara eeh, pamoja na Maria Halimoja, hawa ni ndugu zake wafanyabiashara kutoka hapa Dodoma. Mnataka muwaone, nafikiri mmewaona, wako pale mmewaona, ahsante sana. Karibuni sana Dodoma, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa wale watakaotaka labda pengine watawasiliana na Mheshimiwa Festo ili waweze kupata muda mzuri zaidi wa kujua biashara hiyo sasa na wao kama wakitaka kujifunza masuala ya biashara kwa sababu Mheshimiwa Festo ni mfanyabiashara, kwa hiyo, watakuwa jirani na wafanyabiashara hawa. *(Kicheko)*

Lakini pia kuna tangazo hapa kutoka kwa Katibu; Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi pamoja na Kamati ya Bajeti mnatangaziwa kuwa leo tarehe 8 Juni, 2021 kutakuwa na kikao na Serikali kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa bajeti ya Wizara. Kikao hicho kitafanyika saa 05:30 asubuhi hii katika Ukumbi wa Msekwa D. Waheshimiwa Wajumbe wote mnaombwa kuhudhuria kikao hicho muhimu bila kukosa na mzingatie muda.

Lakini pia Mheshimiwa Seif Gulamali, Mbunge na Meneja wa *Bunge Sports Club* ametuletea tangazo kwamba Jumamosi kutakuwa na bonanza kati ya Bunge na *CRDB.* Na michezo itakayokuwepo ni pamoja na *football, netball, volleyball, basketball* na kuvuta kamba kwa hiyo, ni vyema tukashiriki wote. *(Makofi)*

Nafikiri na huu mchezo wa kuvuta kamba, Mheshimiwa Antipas anauratibu vizuri kabisa. Kwa hiyo, tujitokeze kwa wingi kwa ajili ya kushiriki kwenye bonanza hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu kwa leo. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 04:15 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 9 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*